© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Swali la 1

Allaah ametuumba kwa sababu gani?

Jawabu

Tumeumbwa (na Allah) ili tumuabudu Yeye pekee na wala tusimshirikishe na kitu chochote.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

Na sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi (Soorah adh-Dhariyaat 51:56)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Haki ya Allaah kwa viumbe vyake ni **kumwabudu Yeye pekee bila ya kumshirikisha na yeyote mwengine**) [Bukhari na Muslim]

Swali la 2

Vipi tumuabudu Allaah?

Jawabu

Kama tulivyo amrishwa na Allaah na Mtume wake

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعْبُدُواْ ٱللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ ۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلْقَيِّمَةِ ﴿٥﴾

Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allaah kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na wasimamishe Sala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini madhubuti (Soorah al-Bayyinah 98:5)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili kutoka kwenye sunnah

(yeyote anaye fanya amali (kitendo chochote kwenye Ibadah – dini) ambayo sisi hatukuamrisha basi itakataliwa) – [sharti kitendo hicho kiambatane na Sunnah] [Muslim]

Swali la 3

Je tumuabudu Allaah kwa khofu na matarajio?

Jawabu

Naam, inatakiwa tumuabudu kwa khofu na matarajio

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَٱدْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا

Na muombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. (Soorah al-A'raaf 7:56)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Namuomba Allaah anipe pepo na najilinda kwake na moto (wa jahanam)) [Abu Dawood]

Swali la 4

Ni nini Ihsaan ?

Jawabu

Ihsaan ni kutambuwa kwamba Allaah anatuona tunapokuwa kwenye ibaadah

Dalili kutoka kwenye Qur'an

ٱلَّذِى يَرَىٰكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٨﴾

Ambaye anakuona (mtume) unapo simama (usiku kwenye salah)
(Soorah ash-Shu'araa 26: 218)

Dalili kutoka kwenye sunnah

([Ihsaan] Ni kumuabudu Allaah kana kwamba unamwona na hata kama humwoni basi kwa hakika Yeye anakuona) [Muslim]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Swali la 5

Kwa nini Allaah alituma Mitume ?

Jawabu

Ili kuwalingania watu wamuabudu Allaah pekee na kukanusha kumfanyia ibaadah kwa asiyekuwa Allaah

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allaah, na muepukeni *Tâghût*. (Soorah an-Nahl 16:36)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Mitume wote ni ndugu na dini yao ni moja) [Muslim]

Swali la 6

Ni nini maana ya Tawheed?

Jawabu

Tawheed nikumuabudu Allaah bila ya kumshirikisha na kitu chochote (kuelekeza Ibaadah zote kwa Allaah) kwa mfano katika dua, nadhiri, hukumu (na ibadah zote nyengine)

Dalili kutoka kwenye Qur'an

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ

Basi jua ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa hakki isipokuwa Allaah (Soorah Muhammad 47:19)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili kutoka kwenye sunnah

(jambo la kwanza utakalo walingania ni: Laa ilaha ila Allaah (hapana apasae kuabudiwa kwa hakki isipokuwa Allaah)) [Bukhari na Muslim]

Swali la 7

Ni nini maana ya hapana Mola ila Allaah (Laa ilaha ila Allaah) ?

Jawabu

Maana yake ni hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allaah

Dalili kutoka kwenye Qur'an

ذَٰلِكَ بِأَنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِۦ هُوَ ٱلْبَٰطِلُ

Hayo ni kwa kuwa Allaah ndiye Wa Kweli, na kwamba wale wanao waomba badala yake, ni baat'ili (mfano sheytan na miungu yote mengine) (Soorah al-Hajj 22:62)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Atakaesema (na kukiri) La ilaha ila Allaah kisha akakanusha ibaadah yoyote kinyume na Allaah basi huyo imeharamishwa mali yake na damu yake , na hisabu yake iko kwa Allaah)) [Muslim]

Swali la 8

Ni nini maana ya Tawheed ya majina na sifa za Allaah?

Jawabu

Ni kuamini na kuthibitisha majina na sifa za Allaah kama vile alivyo eleza Allaah kwenye kitabu (Qur'an) chake na alivyo eleza Mtume katika sunnah saheeh.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

لَيْسَ كَمِثْلِهِۦ شَىْءٌ ۖ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ ﴿١١﴾

Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona. (Soorah ash-Shooraa 42:11]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Allaah huteremka (kwenye wingu ya chini) kila siku wakati wa usiku). [Ahmad]

Swali la 9

Ni nini manufaa ya Tawheed kwa muislamu?

Jawabu

Uongozi na kuwa kwenye njia ya kunyoka duniani na kuepuka na adhabu ya moto akhera.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَلَمۡ يَلۡبِسُوٓاْ إِيمَٰنَهُم بِظُلۡمٍ أُوْلَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلۡأَمۡنُ وَهُم مُّهۡتَدُونَ ﴿٨٢﴾

Wale ambao wameamini (na tawheed)**, na hawakuchanganya imani yao na dhulma** (shirk – kuabudu asiekuwa Allaah) - **hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka.** (Soorah al-An'aam 6:82)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(haki ya viumbe juu ya Allaah ni kuwa Hatomuadhibu yule asiyemshirikisha Allaah na chochote) [Bukari na Muslim]

Swali la 10

Allaah yuko wapi?

Jawabu

Allaah yuko juu ya 'Arsh Yake ambayo iko juu ya wingu ya saba.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

ٱلرَّحۡمَٰنُ عَلَى ٱلۡعَرۡشِ ٱسۡتَوَىٰ ﴿٥﴾

Kisha Akapaa juu ya 'Arsh (kwa njia inayolingana na Utukufu wake) (Soorah Taa Haa 20:5)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Allaah aliandika kwenye kitabu alicho nacho Mwenyewe juu ya 'Arsh kwamba Rehma yake ime takadamu (imetangulia au imeshinda) Hasira Yake) [Bukhari]

Swali la 11

Je Allaah yuko nasi kwa elimu yake?

Jawabu

Allaah yuko nasi kwa elimu yake, yuwatuona na anatusikia

Dalili kutoka kwenye Qur'an

قَالَ لَا تَخَافَآ إِنَّنِى مَعَكُمَآ أَسۡمَعُ وَأَرَىٰ ﴿٤٦﴾

Akasema (Allaah): Msiogope! Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na ninaona (Soorah Taa Haa 20:46)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(munamuomba Yule ambaye Anawasikiya na yuko karibu nanyi) [Muslim]

Swali la 12

Dhambi gani ndiyo (a'dhaam) kubwa kuliko zote?

Jawabu

Dhambi iliyo kubwa kuliko zote ni (Shirkul Akbar - shirki kubwa) nayo ni kumshirikisha Allaah.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

إِنَّهُۥ مَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدۡ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِ ٱلۡجَنَّةَ وَمَأۡوَىٰهُ ٱلنَّارُۖ

Kwani anaye mshirikisha Allaah, hakika Allaah atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. (Soorah al-Maaidah 5:72)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili kutokana kwenye sunnah

(Mtume aliulizwa: dhambi gani ni kubwa kuliko zote? Naye akajibu kwa kusema; Kumshirikisha Allaah na japo Yeye ndiye Aliye kuumba) [Bukhari]

Swali la 13

Ni nini Shirkul Akbar (shirki kubwa)?

Jawabu

Nikuelekeza Ibaadah yeyote kwa asiye kuwa Allaah (kumuabudu yeyote mwengine asiyekuwa Allaah)

Dalili kutoka kwenye Qur'an

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغۡفِرُ أَن يُشۡرَكَ بِهِۦ وَيَغۡفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ

Hakika Allaah hasamehe anapo shirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakae. (Soorah an-Nisaa 4:48)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(dhambi zilizo kubwa ni: Shirki (kumshirikisha Allaah) nk. (mpaka mwisho wa hadithi)) [Muslim].

Swali la 14

Ni yapi madhara ya Shirkul Akbar (shirki Kubwa)

Jawabu

Ndio sababu ya mtu kutiwa motoni milele.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

إِنَّهُۥ مَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدۡ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِ ٱلۡجَنَّةَ

Kwani anaye mshirikisha Allaah, hakika Allaah atamharimishia Pepo (Soorah al-Maaidah 5:72)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili kutoka kwenye sunnah

(yeyote anaye kufa hali alikuwa anamshirikisha Allaah ataingiya motoni) [Muslim]

Swali la 15

Je amali njema zita wanufaisha wale wanao mshirikisha Allaah?

Jawabu

Amali njema hazito wanufaisha wale wanaomshrikisha Allaah.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَلَوْ أَشْرَكُوا۟ لَحَبِطَ عَنْهُم مَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿٨٨﴾

Na lau wangelimshirikisha (Allaah) yangeliwaharibikia waliyo kuwa wakiyatenda (Soorah al-An'aam 6:88)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Yeyote anaye tenda amali na akanishirikisha mimi (akaelekeza hiyo amali kwa mwingine asiye kuwa Allaah) nitamkataa yeye na kitendo chake) [Muslim]

Swali la 16

Je vinapatikana vitendo vya shirki miongoni mwa Waislamu katika zama hizi?

Jawabu

Ndio vinapatikana.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُم بِٱللَّهِ إِلَّا وَهُم مُّشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾

Na wengi katika wao hawamuamini Allaah pasina kuwa ni washirikina (Soorah Yoosuf 12:106)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Haitosimama siku ya qiyamah mpaka makabila kutoka Ummah wangu (wa ki-Islamu) watawaiga mushirikina kwa kuabudu masanamu) [Tirmidhi]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Swali la 17

Ni nini hukmu ya mtu kuomba dua (kumuomba) mwengine asiyekuwa Allaah mfano kumuomba mtu aliye kufa?

Jawabu

Kuomba dua (kumuomba) kwa mwengine asiyekuwa Allaah ni shirk-ul-akbar (shirki kubwa).

Dalili kutoka kwenye Qur'an

فَلَا تَدْعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ فَتَكُونَ مِنَ ٱلْمُعَذَّبِينَ ﴿٢١٣﴾

Basi usimuombe mungu mwengine pamoja na Allaah ukawa miongoni mwa watakao-adhibiwa. (Soorah ash-Shu'araa 26:213)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Yeyote anaye kufa na akawa amemuomba mwengine asiyekuwa Allaah ataingia motoni) [Bukhari]

Swali la 18

Je kuomba Dua ni Ibadah?

Jawabu

Ndiyo kuomba Dua ni Ibadah

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدْعُونِىٓ أَسْتَجِبْ لَكُمْ

Na Mola wenu anasema: Niombeni nitakuitikieni. (Soorah Ghaafir 40:60)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Dua ni Ibadaah) [Tirmidhi]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Swali la 19

Je waliyo kufa wanazisikia dua zetu?

Jawabu

La, waliyo kufa hawasikii.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَمَآ أَنتَ بِمُسْمِعٍ مَّن فِى ٱلْقُبُورِ ﴿٢٢﴾

Wala wewe si wa kuwasikilizisha walio makaburini. (Soorah al-Faatir 35:22)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Allaah ameweka malaika ili wanieleze ninapo tumiwa salamu na Ummah wangu) [Ahmad]

Swali la 20

Je twaweza kuomba nusra kwa wale walio kufa ama wale wasio kuwepo?

Jawabu

Haitakiwi tuombe kutoka kwao, bali tunatakiwa tuombe msaada kutoka kwa Allaah.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَٱسْتَجَابَ لَكُمْ

Mlipo kuwa mkimuomba maokozi Mola wenu, naye akakujibuni. (Soorah al-Anfal 8:9)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Ewe Uliye hai milele, Msimamizi wa mambo yote, nakuomba msaada kutokana na Rehma yako) [Tirmidhi]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Swali la 21

Je inaruhusiwa mtu kuomba usaidizi kutoka kwa asiyekuwa Allaah?

Jawabu

La hairuhusiwi.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ۝٥

Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada (Soorah al-Faatihah 1:5)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(na ukiomba muombe Allaah, na ukitaka msaada basi mtake msaada Allaah) [Timidhi]

Swali la 22

Je twaweza kuomba usaidizi kwa wale waliohai?

Jawabu

Ndiyo tunaruhusiwa katika vitu ambavyo wana uwezo wa kutusaidia.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ

Na saidianeni katika wema na uchamngu. (Soorah al-Maaidah 5:2)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Allaah humsaidiya mja maadamu mja anamsaidiya nduguye (Muislamu)) [Muslim]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Swali la 23

Je inaruhusiwa kuweka nadhiri kwa mwengine asiyekuwa Allaah?

Jawabu

La hairusihwi kuweka nadhiri ila kwa jina la Allaah peke.

Dalili kutoka kwenye Qur'an

رَبِّ إِنِّي نَذَرْتُ لَكَ مَا فِي بَطْنِي مُحَرَّرًا

Mola wangu! Nimekuwekea nadhiri kilichomo tumboni mwangu kuwa wakfu (Soorah al-'Imraan 3:35)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Yoyote anayeweka nadhiri kumtii Allaah basi na amtii, na yoyote anaye weka nadhiri kumuasi Allaah basi asimuasi) [Bukhari]

Swali la 24

Jee inaruhusiwa kuchinja (dhabiha) kwa jina isiokuwa ya Allah?

Jawabu

Laa hairuhusiwi.

Dalili kutoka kwa Qur'an

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ ﴿٢﴾

Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako (pekee) (Soorah al-Kawthar 108:2)

Dalili kutoka kwenye sunnah

(Allah anamlaani kila anaye chinja dhabiha kwa jina isiokuwa ya Allah) [Muslim]

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Suali la 25

Jee inaruhusiwa kutufu kwenye makaburi ya watu wema (walio kufa)?

Laa hairuhusiwi.

Dalili kutoka kwa Qur'an



Na watufu nyumba ya kale (Ka'bah) (Soorah al-Hajj 22:29)

Dalili kutoka kwa sunnah

(Yeyote anaye tufu nyumba (Ka'bah) mara saba na akasali rakaa mbili …) [Ibn Majah]